


# MAHUSIANO YETU TANO (5) NA MUNGU:

## UHUSIANO WA KWANZA; "KIUMBE KWA MUUMBA"

Ninakusalimu asubuhi ya leo. Natumai u buheri wa afya katika Kristo Yesu.

Katika Chapisho lililopita tulielezea mahusiano yetu 5 na Mungu:
- Kiumbe kwa Muumba
- Mtumishi kwa Bwana Wake
- Rafiki kwa Rafiki
- Mtoto/Mwana kwa Baba
- Mchezaji kwa Kocha

Wiki hii ningependa tuzungumzie maana ya kuwa kiumbe aliyeumbwa na Mungu wa Biblia- Muumba wa vitu vyote vilivyopo.

Ulimwengu wa kilimwengu/kidunia/kimataifa umemwondoa Mungu Wa Biblia kama muumbaji, katika nia ya kuelewa sisi ni nani na tunakotoka kama wanadamu.

Mwanadamu wa kisasa anaamini kuwa hatujaumbwa kwa mfano wa Mungu, wala hatuna roho ya kibinadamu. Kwamba wanadamu waliibuka kutoka kwa mabilioni ya miaka ya mageuzi duniani - kutoka kwa viumbe tofauti na kufanyika wanadamu wa kisasa.

Kuamini hivi kunamaanisha kuwa tunaishi kama viumbe vya asili bila maana, bila kusudi na bila hatima ya milele. Tunaishi tu mpaka tupitwe na Kifo kwenye barabara kuu ya maisha, kufutiliwa mbali, na kutupwa kwenye shimo la historia ambayo itasahaulika hivi karibuni.

Tulifikaje mahali kama hapa? Ni hadithi ndefu inayoanzia hapo mwanzo.

Biblia inatuambia sisi ni viumbe vilivyoumbwa na Mungu kuwa sehemu ya utaratibu wa kiasili. Ni lazima kula na kulala. Tunahitaji mavazi na makazi. Tunaoana na kuzaa watoto. Lakini katika hali yetu ya sasa, tunang'ang'ana kuishi. Tunaugua. Tunazeeka. Tunakufa.

Lakini Mungu alituumba tuwe zaidi ya hivi! Soma MWANZO 1-3. Mungu alituumba tuwe viumbe vya asili isiyo ya kawaida. Alituumba ili tuishi katika ulimwengu wa asili na pia ulimwengu wa kiroho kwa wakati mmoja. Alituumba ili tuishi katika uhusiano naye.

Mungu alituumba tuishi Edeni: bila magonjwa, bila majeraha, bila njaa, bila hofu, bila kuzeeka, bila kifo.

Lakini kuna kitu kilienda vibaya sana!

Adamu na Hawa waliukubali uwongo wa kwamba wangeweza kupata maisha bora zaidi kwa kujitegemea, kutengana na Muumba wao na kuishi maisha kwa masharti yao wenyewe.

Wakristo wanaliita jambo hili "Anguko". Walianguka kutoka katika muundo wao ulioumbwa na Mungu. Walianguka kutoka katika uhusiano wao na Mungu. Walianguka kutoka kwa wito wao mkuu zaidi wa kuitawala dunia. Walianguka kutoka katika nafasi zao za mamlaka. Walianguka kutoka mahali pao peponi.

Paulo anaiweka hivi:

**WARUMI 5:12** *'Kwa njia ya mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, nayo ikasababisha kifo. Hivyo kifo kimeenea katika jumuiya yote ya binadamu, kwa maana wote wametenda dhambi.'*

**WARUMI 3:23** *'...kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu'*

Sasa umetambua hali hii. Kama viumbe ambavyo kila mmoja wetu ameshiriki kwa njia yake katika janga hili la kutisha kwa kujaribu kuishi maisha kwa masharti yetu wenyewe; kwa kujaribu kuishi maisha mbali na uhusiano wenye upendo na utiifu pamoja na Muumba wetu.

Na matokeo yake ni mabaya;

**WARUMI 6:23** *'Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.'*

Mungu alituumbia umilele. Kwa hivyo ni nini hufanyika tunapokufa kama viumbe vya asili mbali na Muumba wetu? Kifo humtoa mwanadamu wa asili katika umilele wake na kumweka katika umilele wa kutisha unaotengana na Mungu na Watu wa Mungu - huu ni umilele katika moto.

Kwa miaka kadhaa nilisaidia kufundisha kambi ya kiroho katika gereza lenye ulinzi mkali kwa wafungwa wapatao arobaini. Wengine walikuwa katika safari ya kiroho. Wengine walikuwa wageni kwa Imani. Baadhi walikuwa wanaendelea kukomaa vyema katika Kristo Yesu.

Ningeuliza kila kundi, “Unaweza kufanya nini ili ujipate Kuzimu?”

Pindi moja, mfungwa mmoja aliinua mkono wake na kujibu, “Uue mtu?” (Unaweza kukisia kilichomtia gerezani.)

“Hakika hilo litakuharakisha,” nikajibu, “lakini hilo si jibu sahihi.”

“Kumbaka mtu?” mfungwa mwingine akajibu. (Unajua alikokuwa anatoka.)

"Tena, sio jibu sahihi, ingawa hilo hakika litasaidia."

"Kutengeneza na kuuza madawa mengi ya kulevya?"

"Nina hakika hilo litakusaidia kufika huko lakini bado sio jibu sahihi.”

Wafungwa hao walinikodolea macho wakisubiri jibu sahihi.

Nikasema, “Jibu ni 'Hakuna'. Hakuna kitu kabisa. Amka kila asubuhi. Ishi maisha kivyovyote na kwa jinsi unayotaka. Hatimaye utakufa na kwenda Kuzimu."

Kila kitu katika ulimwengu wa asili kina mpangilio wa kimsingi: jua huchomoza na kutua - makundi ya wanyama katika mbuga ya Serengeti huhama na kurudi - mawimbi ya pwani huingia na kutoka. Tukiwa viumbe wa kibinadamu wanaoishi kando na Muumba wetu, mpangilio wetu wa kimsingi utakuwa ni kuzaliwa - kuishi - kufa - kuishia Kuzimu milele.

Lakini hivi SIVYO ambavyo Muumba wetu alikusudia kwa ajili yetu. Hilo silo tamanio la Muumba wetu kwetu. Hilo sio chaguo letu la pekee.

Katika chapisho letu linalofuata tutazungumzia jinsi tunaweza kuianza safari ndefu ya kuirudia asili yetu halisi. Jinsi tunavyoweza kurejesha uhusiano uliopotea kati yetu na Muumba wetu. Jinsi tunaweza kugundua maisha - Maisha ya Kweli.

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.

Ni wako

Douglas

Douglas Van Devender.

Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.